OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA

EINOTI HIGH SCHOOL
S.L.P 15018,
ARUSHA
**E-mail** einotisecondaryschool@gmail.com:**website**:www.einotisecschool.ac.tz

**Kumb.Na.ESS/AB/VOL.1/03**

Simu: 0758086958 Mkuu wa shule.

0754552163/0754523307, Makamu mkuu wa shule

0759407476/0629080833, Matron.

0787969045, Patron.

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi.
…………………………………….
S.L.P………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI EINOTI. HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA MKOA WA ARUSHA MWAKA 2023.**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2023 tahasusi ya **HGK.**

Shule ya Sekondari EINOTI ipo umbali wa kilomita 5 Kaskazini Magharibi mwa mji mdogo wa Kisongo Arusha. Ukifika kituo cha mabasi Mkoani Arusha panda hiace zinazoenda Kisongo hadi mwisho wa hiace, nauli yake ni Tsh.700/= ukifika Kisongo kuna usafiri wa bodaboda kwa Tsh. 2000/= hadi Einoti Sekondari.

Aidha siku za kufungua na kufunga Shule huduma ya usafiri wa hiace pia unatolewa kwa gharama hizo hizo.

Muhula wa masomo unaanza tarehe **14/08/2023** na kila mwanafunzi atatakiwa kuripoti shuleni ndani ya wiki mbili na si vinginevyo.

*SCHOOL MOTTO: “EDUCATION FOR DEVELOPMENT”*

**2: Mambo muhimu ya kuzingatia.**

**2.1: Sare ya Shule.**

**A.WASICHANA**

a}Sketi mbili za kitambaa rangi ya VICTORY namba 31 ndefu inayopita magoti ikiwa na mshono wa Rinda Box mbele na nyuma.
b} Tai moja (1) rangi ya Victory namba 31.
c}Mashati mawili meupe ya mikono mirefu .
d} Sweta jeusi la V lenye mistari meupe shingoni.
e} Tshirt ya shule bluu bahari form six yenye mistari meusi shingoni
f} Suruali mbili (2) za rangi ya VICTORY zitavaliwa ndani ya sketi.
g} Viatu vya ngozi jozi mbili (2) vyenye gidamu (vya kufunga kamba) na visiwe na kisigino kirefu
h} Soksi nyeupe ndefu jozi mbili(2).
i} Gauni la kushindia kitambaa cha draft mshono wa solo ( Masai yenye mistari nyeupe na kijani)
j}Suruali ya kushindia ndani ya gauni akipenda (rangi ya kaki).
k} Trucksuit ya rangi ya maruni yenye mistari meupe.
l} Raba jozi moja(1) rangi nyeupe flat kwa ajili ya michezo.
m}Hijabu nyeupe isiyo na urembo (kwa waislamu tu)
n} Nguo za ndani za kutosha

**B.WAVULANA**

a} Suruali mbili za kitambaa rangi ya VICTORY namba 31 ndefu inayofunika kisigino cha mguu yenye turn up,mfuko mmoja nyuma ,na pembeni kulia na kushoto mmoja mmoja.
b} Tai moja (1) rangi ya Victory namba 31.
c} Mashati mawili meupe ya mikono mirefu .
d} Sweta jeusi la V lenye mistari meupe shingoni
e} Tshirt ya shule bluu bahari form six yenye mistari meusi shingoni.
f} Viatu vya ngozi jozi mbili (2) vyenye gidamu (vya kufunga kamba) na visiwe na kisigino kirefu
g} Soksi nyeusi jozi mbili(2).
h} Suruali ya kushindia rangi ya kaki ndefu mpaka kwenye kisigino.
j} Trucksuit ya rangi ya maruni yenye mistari meupe.
k} Raba jozi moja(1) flat rangi nyeupe kwa ajili ya michezo.
n} Nguo za ndani za kutosha

**NB:Mwanafunzi asije na nguo yoyote tofauti na sare zilizoagizwa.**

**2.2: VITU MWANAFUNZI ANAVYOTAKIWA AJE NAVYO SHULENI.**

i} Result slip (kivuli).
ii} File/jalada dogo(spring file) la kutunzia mitihani rangi ya kijani.
iii} Madaftari saba (7)counter,mathematical set na kalamu.
iv}Godoro la futi 2.5 lenye cover(kitambaa).
v} Mito na foronya rangi ya(bluu bahari) kwa wanafunzi wa kiume na ( pink) kwa wanafunzi wa kike.
vi} Shuka mbili (bluu bahari) na blanket moja zito kwa wanafunzi wa kiume na (pink) kwa wanafunzi wa kike.
vii} Ndoo mbili (2) za lita kumi (10) kwaajili ya usafi binafsi.
viii} Rimu moja (1) kwaajili ya photocopy ($A_4$) na rimu moja yenye mistari (rulled) kwaajili ya mazoezi
ix} Orodha ya vitabu kwa tahasusi yake,imeambatanishwa nyuma ya fomu hii
x} Vyombo vya chakula (Sahani,bakuli, kikombe na kijiko).
xi} Vifaa vya usafi; soft broom moja(1),ufagio wa chelewa mmoja(1) na Jembe moja (1)na mpini wake.

**2.3: Simu za mkononi na line haziruhusiwi kabisa.**
i}Kutakuwa na ukaguzi siku ya kuripoti shuleni na ukaguzi wa dharura wakati wowote mwanafunzi akiwa shuleni.
ii} Mzazi atoe namba yake ya simu kwa mawasiliano ya haraka kupitia ofisi ya mkuu wa shule na katika fomu ya maelekezo binafsi iliyoambatanishwa.
iii} Mwanafunzi atakayekamatwa na simu, **''ATAFUKUZWA SHULE''**.
2.2.3} Mwanafunzi atakabidhi stamp na anuani inayopatikana kwa ajili ya kutuma fomu ya maendeleo kwa mzazi wake (PRF) kila muhula wa masomo.
**2.2.4 FORM YA AFYA.**
Hapa imeambatanishwa fomu ambayo lazima Daktari wa Hospitali ya umma (Serikali) aijaze kwa kumpima mwanafunzi husika,kusaini katika fomu na kuweka muhuri kuthibitisha taarifa husika
(**Isiwe kituo cha afya**).Taarifa hii ya afya ya mwanafunzi itatusaidia kumhudumia mwanafunzi husika awapo shuleni.
**2.2.5: Unatakiwa kuja na nakala ya cheti cha kuzaliwa (Birth certificate) au kitambulisho cha taifa (ni lazima)**
**2.2.6: Kukubali masharti ya shule.**
Pamoja na barua hii imeambatanishwa sheria za shule na fomu ya kukubali sheria hizo na mkataba wa kutoshiriki katika migomo,fujo na makosa ya jinai.Unachotakiwa kufanya ni kusoma sheria hizo kwa makini na kuweka saini yako katika fomu ya kukubali kujiunga na shule hii,iwapo umekubaliana na masharti yaliyotajwa.
**2.2.7: Shule hii ni ya serikali hivyo haina dini.**
Kwa mwanafunzi mwenye msimamo mkali wa dini,mzazi anashauriwa ampeleke shule za seminari.Mzazi/mlezi anaruhusiwa kuja shuleni kumsalimia mwanafunzi wake,kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi**. Kamwe mtu asiye mzazi/mlezi haruhusiwi kumtembelea mwanafunzi.**
**2.2.8.Mwanafunzi haruhusiwi kuwa nje ya shule (mjini) pasipokuwa na ruhusa kutoka kwa mkuu wa shule.**)

**2.2.9. MICHANGO**
**Kila mzazi atawajibika kuchangia maendeleo ya shule kwa michango ifuatayo:**
1. **ADA : Hakuna malipo ya ada kwa kuwa Serikali imegharamia.**
2. **Tshs 65,000/= kwa mwaka gharama za uendeshaji wa shule**
3. **Tshs 5,000/= Tahadhari**
4. **Tshs 5,000/= Nembo**
5. **Tshs 5,000/= Kitambulisho cha shule**

**NB: MICHANGO YOTE ILIPWE KUPITIA AKAUNTI YA SHULE NMB 40801200250 EINOTI SEKONDARI**
**Kila mwanafuzi aje na Bima yake ya afya, iwapo huna utatakiwa kulipia bima hiyo Tsh. 6000/= kwa mwaka. (Lazima)**
**3.0:** Mwanafunzi atatakiwa kurudi kwa mzazi au mlezi wakati wa likizo fupi au ndefu. Hivyo mzazi unapaswa kumtumia mwanao nauli mapema.
**NB: i}** Vitu vya gharama kama vile Kamera,Heater,TV,computer, radio na vinavyofanana na hivyo **haviruhusiwi** hapa shuleni.
**ii}** Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na **pay-in-slip** za malipo ya shule,michango yote na vifaa vyote.

Nakutakia safari njema kuja hapa Einoti
***Karibu sana!***

……………………………………………………….
**Justine R. Swai.**
**MKUU WA SHULE**

**Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa Shule.**

a) Wizi
b) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
c) Uasherati, ushoga, kusagana na ubakaji
d) Kupata au kusababisha mimba.
e) Kutoa mimba au kusaidia kutoa mimba.
f) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
g) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi,cocaine,mirungi,kuberi,na kadhalika.
h) Kupiga au kupigana.
i) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
j) Kudharau bendeara ya Taifa.
k) Kuoa au kuolewa.
l) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa Shule au Watu.
m) Kukataa adhabu kwa makusudi.
n) Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
o) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
p) Kutembelea katika majumba ya starehe na Nyumba za kulala wageni.
q) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu;

**SHERIA ZA SHULE.**

Taarifa njema ni ya lazima na inatiliwa mkazo hapa Shuleni.Mwanafunzi mwenye tabia mbaya hafai kupewa Elimu ya sekondari au Elimu ya juu.Ni lazima mwanafunzi awe na tabia nzuri wakati wote.Kila mwanafunzi analazimika kutii sheria za shule na kufuata taratibu za shule,pia kuwatii wafanyakazi wa shule , walimu na wengine wenye mamlaka. Heshima na adabu kwa mtu yeyote ni kitu cha lazima.

1) Kunywa pombe au kuvuta sigara au kiko ni mwiko.
2) Uasherati ni kosa kubwa sana.
3) Kila mwanafunzi ni lazima awe mtiifu kwa walimu wake wote , wafanya kazi wasio walimu na wanafunzi wenzake wote wa kike na kiume.Ujeuri au ubishi wa aina yoyote kwa walimu,wafanyakazi wasio walimu au kwa wanafunzi wengine ni mwiko.
4) Hakuna mwanafunzi yeyote anayeruhusiwa kutoka nje ya mipaka ya maeneo ya shule bila ruhusa (pass) toka kwa mwalimu wa zamu,isipokuwa siku ya kuruhusiwa kwenda mjini rasmi (town leave).Mwalimu akimwona mwanafunzi yeyote mjini anawajibu wa kumuuliza amwonyeshe cheti cha ruhusa (pass).
5) Ruhusa ya kulala nje ya Shule inatolewa na mkuu wa shule au makamu mkuu wa shule tu.
6) Kila mwanafunzi lazima aheshimu kazi za mikono zote ikiwa ni pamoja na bustani,usafi kama vile anavyopaswa kuheshimu masomo ya darasani.
7) Matusi ya aina yoyote,yawe ya kusema au ya kuandika hayaruhusiwi shuleni.
8) Kila mwanafunzi lazima aheshimu na kutunza mali ya shule,uharibifu wowote utakaotokea utabidi ugharamiwe na mwanafunzi mwenyewe.
9) Sare za Shule (Uniform) ni lazima zivaliwe wakati wa masomo na wakati wa kuruhusiwa kwenda mjini. Hakuna mwanfunzi yeyote atakayeruhusiwa kutoka nje ya mipaka ya shule bila kuvaa sare za shule,isipokuwa tu kama ruhusa rasmi imetolewa na mkuu wa shule.
10) Wizi wowote hauruhusiwi shuleni,iwe ni wa mali ya shule au mali ya mwanafunzi au mfanyakazi yeyote.

11) Ugomvi wa maneno au kupigana ni mwiko shuleni.
12) Usafi wa mwili ,mavazi,madarasa,mabweni,Bwalo (Dining hall) na viwanja vya shule ni wajibu wa kila mwanafunzi
13) Kuchelewa kwa aina yoyote bila ruhusa ni kosa,mfano kuchelewa toka mjini wakati wa roll-call,kuchelewa inspection na kuchelewa toka likizo.
14) Tabia njema shuleni, na nje ya shule ni wajibu na lazima kwa kila mwanafunzi.
15) Taa za shule na maji ya shule ni lazima zitumiwe kwa uangalifu mkubwa sana.
16) Magazeti au vitabu vyenye picha au maneno yasiyofaa havitakiwi shuleni.
17) Upokeaji au uandishi wa maneno yasiyofaa ni mwiko shuleni.
18) Mwanafunzi yeyote haruhusiwi kuandika barua yeyote kwa mkuu yoyote mahali popote ya kiofisi bila ya kuipitisha kwa mkuu wa shule (k.k Mkuu wa shule).
19) Mwanafunzi yeyote haruhusiwi kwenda nyumbani kwa Mwalimu au Mfanyakazi yeyote bila ruhusa ya mwalimu anayehusika.
20) Mwanafunzi yeyote haruhusiwi kutumia vyombo vinavyotumia umeme kama vile redio,heater,pasi,mabwenini au kufanya ufundi wa aina yoyote kwenye mfumo wa umeme bwenini au madarasani.
21) Kila mwanafunzi ni lazima ahudhurie vipindi vyote vya madarasani pamoja na "night preparation".
22) Ni kosa kupiga kelele hovyo shuleni.
23) Ni kosa kugomea mitihani ya ndani au ya nje.
24) Ni kosa kugomea chakula cha shule.
25) Ni kosa kwa mwanafunzi yeyote kufanya marekebisho kwenye sare ya shule.
26) Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.
27) Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

……………………………
…………………………….
Tarehe…………………….

Mkuu wa shule,
Einoti Sekondari,
S .L.P. 15018,
**ARUSHA.**

YAH: **KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI EINOTI**.

Nachukua nafasi hii kulishukuru Taifa kwa kunichagua na kunipa nafasi ya kupata Elimu ya sekondari ya juu. Hii ni bahati kubwa na ninaahidi kijifunza kadiri ya uwezo wangu na sitapoteza muda wa masomo darasani au muda wa kazi za mikono Kwa kuwa mvivu, au kupunguza shughuli hizo.

Nimesoma sheria za shule na masharti ya kujiunga na shule ya sekondariEinoti na ninakuthibitishia kuwa nimeafikiana na sheria na masharti hayo na kwamba nitaziheshimu kwa kutozivunja kwa makusudi.

**Wako mwanafunzi mtiifu,**
**Saini ya mwanafuzi**
**…………………………………….**
**Jina la mwanafunzi**
………………………………………
NB: Wasilisha fomu hii kwa Makamu Mkuu wa Shule mara tu ufikapo shuleni ili iwekwe kwenye jalada lako.

**MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI**

Ikiwa mwanafunzi na mlezi/mzazi watakubaliana na masharti yote ya shule,sharti fomu hii isainiwe na watu watatu, ambao ni:

(i) Mwanafunzi mwenyewe: Jina kamili_______________Kidato ________ Saini __________ Tarehe________

(ii) Mzazi/Mlezi: jina kamili __________________ Saini__________Tarehe ___________

(iii) Mtendaji wa Kata___________________________

Jina la Afisa Mtendaji wa Kata______________________________

Saini ya Mtendaji Kata______________________________Tarehe_____________

Muhuri wa Afisa Mtendaji wa Kata:

Namba ya simu …………………………

NB: Wasilisha fomu hii kwa Makamu Mkuu wa Shule mara tu ufikapo shuleni ili iwekwe kwenye jalada lako.

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA

**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT.**
**(To be completed by a medical Officer in respect of all form 1 and 5 entrants)**

Pupil's full name:……………………………… ……………………………………………..

Age:……………………………………………………………………………………………

Blood count (red and white)……………………………………………………………………

Stool examinations:………………………………………………………………………………

Urinalysis:……………………………………………………………………………………….

Syphilis test:……………………………………………………………………………………..

T.B.Test:…………………………………………………………………………………………

Eye test:…………………………………………………………………………………………

Ears:……………………………………………………………………………………………

Chest:…………………………………………………………………………………………

Abdomen:……………………………………………………………………………………....

Spleen:…………………………………………………………………………………………..

Additional information e.g. Physical defects, infection, chronic or family diseases etc.
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………

I certify that the above is fit to pursue further studies.
Signature………………………………….
Designation……………………………….
Station……………………………………
Date:…………………………………….

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA

---

**SHULE YA SEKONDARI EINOTI**
**FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI.**

1. JINA…………………………………………DINI……………………
2. TAREHE YA KUZALIWA……………..……..3. KIJIJI ULIMO ZALIWA…………..…………...
4. TARAFA ULIMOZALIWA…………….. 5. WILAYA ULIMOZALIWA…………………………
6. MKOA ULIMOZALIWA……………………..… KAMA UNAKAA MJINI…….…..……………
7. TAJA MJI………….……..….MTAA…..……………………..BARABARA………..………….
8. JINA LA BABA………………………………..…9. KAZI YA BABA…………..……………….
10. NAMBA ZA SIMU YA BABA………………………………………..
11. JINA LA MAMA…………………………………12. KAZI YA MAMA…………………………
12. NAMBA ZA SIMU YA MAMA………………………………………….
13. JINA LA ATAKAYEHUSIKA NA MWANAFUNZI KIPINDI CHOTE CHA MASOMO
    JINA……………………………………… ANWANI ……………………….
    SIMU……………………………………….EMAIL………………………..
14. SHULE YA MSINGI ULIYOSOMA …………………………………………………...
    SHULE YA SEKONDARI ULIYOSOMA ………………………………………………
    MADARAKA ULIYOSHIKA...............................................................................................................
15. JE, BABA YU HAI?...............................................................(NDIO/ HAPANA)
16. JE, MAMA YU HAI?...............................................................(NDIO/HAPANA)
17. JE,UNAKAA NA MLEZI………………………………….(NDIO/HAPANA)
18. ANWANI YA MLEZI………………………………………...
19. KAZI YA MLEZI…………………………………………...
20. ELEZA MATATIZO YA NYUMBANI ,N.K YANAYOKUKABILI
    ……………………………………………………………………………………………..
21. UNAFIKIRI MATATIZO HAYO VIPI?...............................................................................
22. ELEZA MIPANGO YA MAISHA YAKO YA BAADAYE…………………………
23. MKO WANGAPI KATIKA FAMILIA? (A) WA KIUME……………………..
    (B) WA KIKE ………………………..(C) WEWE NI NGAPI ?.......................
    (D) NDUGU WANGAPI WAMEAJIRIWA?.........................................................

25.KAZI AMBAZO UNGEPENDA KUFANYA BAADA YA MASOMO…………………...
26. KAZI AMBAZO USINGEPENDA KUFANYA BAADA YA MASOMO……………..
27. JINA…………………………………SAINI…………………..TAREHE………………

NB: Wasilisha fomu hii kwa Makamu Mkuu wa Shule mara tu ufikapo shuleni ili iwekwe kwenye jalada lako la siri.

**ORODHA YA VITABU UNAVYOSTAHILI KUNUNUA.**

**KWAHILI 1.**

**1.** *Historia na matumizi ya Kiswahili*’’ **by Mbunda Msokile 1992**
**2.** *Historia ya usanifishaji wa Kiswahili’’* **by Ireri Mbabu 1991.**
**3.** *Kamusi kuu ya Kiswahili sanifu***by BAKITA.**
**3. Kamusi ya Kiswahili Sanifu (TUKI).**

**KISWAHILI 2.**

**1.** *Fasihi* **by Senkoro F**
**2. ‘***Kunga za fasihi na Lugha***” by Mbunda Msaokile 1992**

**HISTORTY 1.**

**1.** ‘Contemporary *historical Events, Advanced Level History one***”(2nd edition 2014) by Mwalimu Shibitali CK Tumaini**
**2. ‘***Essential in advanced level History***” History ONE (current syllabus) by Saleh Yassin**
**3. ‘***How Europe underdeveloped Africa’’***by Walter Rodney**

**HISTORY 2**

1. *Contemporary historical Events, Advanced Level History TWO* **(2ndeddition 2014) by Mwalimu Shibitali CK Tumaini**
2. *Essential in advanced level History***History TWO (current syllabus) by Saleh Yassin**
3. *‘Basic themes in European Advanced level* **history form 5&6, 2nded 2014. By Ismail Ngobi.**
4. *Mastering history two* **by mwalimu Carte.**

**GENERAL STUDIES**

*1. Understanding Advanced level* **by Joanne BigirwaMungu, based on New syllabus 2010**
**2.** *General studies for Advanced level certificate form "5&6’’* **by Richard Mbalase**

**GEOGRAPHY 1**

Zisti Kamili.*New physical geography* 3rdEd.2016 , kamili bookshop and general supply.
Zisti Kamili.*Practical geography*2016, kamili bookshop and general supply**.**

**GEOGRAPHY 2**

Zisti Kamili. 2016. *Human economic geography*, Kamili bookshop and general supply.
D. T. Msabila. 2017. *Human economic geography*, Nyambari Nyangwine publisher.
John Ezra & Ester Luke. 2017. *Geography two review*. APE network.
Ester Luke & Odemari Rogati. 2016. *Geography review*. APE network.

1. **Viambatanisho na Fomu Muhimu**

   i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
   ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
   iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
   iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

2. **Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu**.

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule ……………………….0717176760**
- **Makamu Mkuu wa Shule ……………0754552163/0682015522**
- **Mwandamizi Taaluma ………………………………0755259349**
- **Mwandamizi Malezi …………………....................0755893293**

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA